

Shikamoo Watumishi wa SPS & Familia,

Kufuatia matukio ya hivi karibuni na wasiwasi mkubwa kuhusu janga la coronavirus (COVID-19) linaloathiri raia wa nchi yetu na kote ulimwenguni, wilaya yetu ya shule inatambua, na inachukua kwa umakini jukumu letu la kuhakikisha usalama na ustadi wa wanafunzi, watumishi, familia na jamii.

Mchana huu Gavana Inslee ametoa hitaji kwa shule za umma zote hapa Serikali ya Washington kufunga mlango kutoka Machi 17 hadi Aprili 24. Wataalam wa afya wanaamini kwamba huu ni uamuzi mzuri wa juhudi za ukali kwa ajili ya kupunguza ueneaji wa virusi ya COVID-19. Tunajua kwamba ufungaji wa shule huu utakuwa na athari kubwa kwenye jamii yetu yote, wanafunzi, familia na watumishi – ambayo ni sababu moja ya kufanya hatua hii kuwa ngumu. Kwa ajili ya kujibu swala hili la tukio ambalo halijawahi kutokea, lengo letu ni kusaidia wanafunzi na familia wakati ambao shule zitakuwa zimefungwa.

Tutakuwa tunatoa vyanzo na vifaa kwa wanafunzi kwa ajili ya kuwasaidia kuendelea kujifunza wakiwa nyumbani. Hii ni pamoja na zana za tovuti na vifaa vingine ambavyo walimu kibinafsi watakuwa wanaweza kutuma nyumbani na wanafunzi. Kuendelea kufanya shughuli za shule wakiwa nyumbani, itawasaidia wanafunzi kukaa macho na kubaki hai hadi shule zifunguwe mlango tena. Kuitikia hali hii kunabadilika, ndiyo sababu tutaendelea kuongeza mipango yetu ya kusaidia wanafunzi mara tu tutakapokuwa na habari mpya.

Shule za Umma hapa Spokane zimeandaliwa kutoa huduma ya Watoto wa watumishi katika majukumu ya utunzaji wa afya, wajibu wa kwanza, na idadi ya watu walio katika mazingira magumu. Pia wanafunzi wote wa SPS watakuwa wanapatiwa chakula.

Maelezo zaidi kuhusu fursa za kuendelea kujifunza kwa wanafunzi, huduma za watoto, na chakula, yanapatikana kwenye tovuti ya wilaya ya shule.

Moyo wa Sokane ni utunzaji tunaonyeshana kama jamii. Wakati huu ushirikiano wetu na viunganisho ni muhimu zaidi kuliko hapo awali tukiwa tunaungana pamoja ili kutafuta ushindi siku za zijazo mbele.

Shelley Redinger
Superintendent
3/13/2020